# MAOMBI

## Ya Kujikuza kiroho

TOLEO LA 8



BY DENIS & DEVIS JULIUS

# MAOMBI  MAALUMU YA KUJIKUZA KIROHO.

## ~Toleo la 8

**UTANGULIZI:**

Karibu katika mwendelezo wa maombi maalumu ya kujikuza kiroho. Kumbuka kuokoka tu peke yake hakutoshi, hatuna budi kukua kiroho, ili tufikie ule utimilifu Yesu aliokusudia sisi tuufikie tukiwa hapa duniani, ili tuweze kushiriki Baraka zote za rohoni Mungu alizotuwekea. Usifurahie kumtumikia Mungu kidini, mfurahie Mungu utakayemwona katika maisha yako ya kila siku. Hupaswi kudhani mchungaji pekee ndio anayeweza kukuombea, na kupokea, unapaswa kujua nguvu ulizonazo ndani yako zinaweza kukuletea majibu yote, bila kumtegemea mwanadamu. Lakini nguvu hizi haziwezi kutoka wakati mwingine bila kujibidiisha katika kufunga na kuomba, ndivyo alivyosema Bwana Yesu(Mathayo 17:21).

Upo mwongozo ambao tunautoa kila mwezi wa ratiba ya mifungo na maombi. Ikiwa utapenda kuupata basi utawasiliana nasi kwa namba zetu zilizo mwisho wa makala hii. Lakini pia ukuaji wa kiroho hutegemea usomaji wa Neno la Mungu. Hivyo basi katika tovuti yetu hii www.wingulamashahidi.org. Utakutana na mafundisho mengi, pamoja na majibu ya maswali wengi ya biblia zaidi ya 4,000. Tembelea utajifunza mengi.

Katika makala hizi tumeegemea zaidi katika eneo la maombi. Mwongozo huu ni wa maombi ya **SAA SITA (6),** Kwa wiki, hivyo kila kipengele unaweza kuombea katika siku moja, labda kwa siku saa moja au mawili. Na ni vema ukaomba hata zaidi ya saa hizo tulizoziorodhesha, kwa ukuaji bora zaidi wa roho yako na wa haraka.

**Zingatia:** Omba katika mazingira ya utulivu wa roho, elekeza mawazo yako kwa Bwana, na kwa jinsi utakavyokuwa unatamka vipengele hivyo, huko huko Kristo naye atakupa kinywa cha maombi utaomba hata zaidi ya hivyo tulivyoviorodhesha, utamfurahia Mungu sana.

Bwana akubariki.

Karibu sasa katika mwongozo wetu..

~Mwl Denis & Devis Julius

# MAMBO SABA (7) YAMPENDEZAYO MUNGU

*Mithali 6:16 Kuna vitu sita anavyovichukia Bwana; Naam, viko saba vilivyo chukizo kwake. 17 Macho ya kiburi, ulimi wa uongo, Na mikono imwagayo damu isiyo na hatia; 18 Moyo uwazao mawazo mabaya; Miguu iliyo myepesi kukimbilia maovu; 19 Shahidi wa uongo asemaye uongo; Naye apandaye mbegu za fitina kati ya ndugu.*

Kama wewe ni mwajiriwa au ulishawahi kuajiriwa, utagundua kuna tabia ambazo ma-boss huwa hawazipendi, mojawapo ya hizo ni kama vile wizi, uvivu, uongo, au kukosa nidhani. Hivyo ikitokea mwajiriwa ameweza kuziepuka, ni wazi kuwa jambo litakalofuata hapo ni yeye kupendwa, kuaminiwa, na hatma yake ni kupandishwa cheo.

Vivyo hivyo na kwa Mungu wetu, zipo tabia nyingi zisizompendeza, lakini ameziandika kuu saba (7), ambazo ikitokea mtu ameziepuka ndani yake, (yaani amefanya bidii kwenda kinyume nazo). Atapendwa kama sio kuaminiwa sana na Mungu, na hatma yake ni kupandishwa daraja la juu sana Rohoni.

Na tabia zenyewe ndio hizi;

1) **Macho ya kiburi**
2) **Ulimi wa uongo**
3) **Mikono imwagayo damu isiyo na hatia**
4) **Moyo uwazao mawazo mabaya**
5) **Miguu iliyo myepesi kukimbilia maovu**
6) **Shahidi wa uongo**
7) **Apandaye mbegu za fitina kati ya ndugu.**

Hivyo katika hizo tutaomba kwa bidii Bwana aziondoe ndani yetu.

## 1. MACHO YA KIBURI (Dk 50)

Kiburi ni hali ya mtu kujiinua aidha kifikra au kimwenendo, na kuamini kuwa yeye yupo juu ya wengine, na kwamba hahitaji msaada wowote kutoka kwa wenzake.

**Zao la kiburi ni;**

I. **Mashindano:** Hupendi kuona mawazo ya wengine yanazidi ya kwako. Yaani Wewe tu ndio uwe juu.

*Mithali 13: 10 Kiburi huleta mashindano tu; Bali hekima hukaa nao wanaoshauriana*

II. **Ukali:** Huna kauli za upole na unyenyekevu.

*Zaburi 10:2 Kwa kiburi chake asiye haki mnyonge anafuatiwa kwa ukali;..”*

III. **<u>Ubishi:</u>** Kutotaka kuelewa, hata kama utaujua ukweli, utaishia kuzua malumbano.

*Mithali 21:24 Mwenye kiburi na kutakabari, jina lake ni mbishi; Hutenda mambo katika majivuno ya kiburi chake.*

IV. **<u>Dharau:</u>** Kuwaona wengine si kitu ukiwalinganisha na wewe.

*Zaburi 123:4 Nafsi zetu zimeshiba mzaha wa wenye raha, Na dharau ya wenye kiburi*

V. **<u>Majivuno:</u>** Kujisifia akili, kipaji, karama, mali . *Zaburi 31:18,*

*VI.* **<u>Kutosikiliza maonyo/ Mashauri:</u>** *Yeremia 13:1*

VII. **<u>Kusema hakuna Mungu:</u>** <u>Kudhani kwamba Mungu hayupo, wala hawezi kuwa msaada ya yoyote</u>

*Zaburi 10:4 Mdhalimu kwa kiburi cha uso wake Asema, Hatapatiliza. Jumla ya mawazo yake ni, Hakuna Mungu*

VIII. **<u>Kuzua Vita:</u>** Ukorofi, na uhasama, ni zao la kiburi. Kuwachokoza wengine.

*Zaburi 56: 2 Adui zangu wanataka kunimeza mchana kutwa, Maana waletao vita juu yangu kwa kiburi ni wengi.*

IX. **<u>Dhaluma:</u>** Kukosa hofu ya kuvitwaa vya wengine, Unaona ni sawa kuwanyima mayatima, au wanyonge haki zao. *Zaburi 119:78*

X. **<u>Visa na mitego:</u>** Zaburi 140: 5 Wenye kiburi wamenifichia mtego na kamba; Wametandika wavu kando ya njia; Wameniwekea matanzi.

**XI.** **<u>Kuzungumza maneno yasiyo na mipaka / yenye mizaha/ yasiyo na staha :</u>**

*Yuda 1:16 Watu hawa ni wenye kunung'unika, wenye kulalamika, waendao kwa tamaa zao, na vinywa vyao vyanena maneno makuu mno ya kiburi, wakipendelea watu wenye cheo kwa ajili ya faida. Soma pia 2Petro 2:18*

Hivyo mwombe Mungu akuondolee tabia hizi, moja baada ya nyingine ndani yako. Unaweza ukadhani hauna kwa kujitazama juu juu, lakini mara nyingi tabia hizi hujificha sana, na zinaamka mahali ambapo zitatibuliwa. Kwamfano huwezi kujijua kuwa wewe una madharau ndani yako, lakini ngoja siku umepata kitu Fulani zaidi ya wengine, labda mali, au fursa au kipawa cha Roho n.k. Utaona tabia hiyo inavyojidhihirisha yenyewe kwa wengine. Hivyo ombea vipengele vyote bila kuacha hata kimoja, kwasababu jicho la Mungu linachunguza sana mioyo yetu.

<u>Kiburi kikiondoka ndani yako, hizi ndio faida utakazozipata;</u>

- ✓ **Kuongezewa neema:** 1Petro 5:5 Vivyo hivyo ninyi vijana, watiini wazee. Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema
- ✓ **Kuepushwa na aibu:** Mithali 11:2 Kijapo kiburi ndipo ijapo aibu; Bali hekima hukaa na wanyenyekevu

## 2) <u>ULIMI WA UONGO.</u> (Dk 50)

Uongo ni silaha-kuu pendwa ya shetani. Bwana Yesu alisema, shetani alikuwa mwongo, tena ndio baba wa huo (Yohana 8:44). Hivyo unapokuwa mwongo, ni moja kwa moja unajitambulisha kuwa baba yako ni ibilisi.

Ulimi wako na moyo wako ni lazima utibiwe na Bwana. Kama Isaya alivyomwomba Mungu, amponye tatizo hilo, Akawekewa kaa la moto kinywani, akaponywa (Isaya 6).

**<u>Hizi ni aina za uongo.</u>**

**I. <u>Kutozungumza ukweli wote. Ni uongo.</u>**

Mfano wa huu ni ule wa Ibrahimu, alipoulizwa juu ya mke wa Sara, akasema ni dada yake. Lakini kiuhalisia ni kweli alikuwa dada yake, lakini pia mke wake. Angepaswa azungumze ukweli wote ili kuepusha mapigo kwa wale wakuu lakini hakufanya hivyo.(Mwanzo 20)

**II. <u>Kuongeza chumvi.</u>**

Ni uongo, unaoongezewa kwenye habari ili kuongeza ukali wa mashitaka. Ndicho walichokuwa wanakifanya wayahudi kwa Bwana Yesu kipindi kile cha kusulubiwa kwake.

**III. <u>Kuficha taarifa ya ukweli</u>**

Uongo huu sio lazima, utamkwe. Lakini upo ndani. Kwamfano Daktari anapoficha kumweleza mgonjwa wake madhara ya utumiaji wa kitu Fulani, na huku akijua kabisa anao wajibu kwa kumwambia ni uongo. Kisha baadaye mtu Yule akaenda kutumia. Tayari Yule daktari kaudhihirisha uongo bila hata ya kuambiwa.

**IV. <u>Kukiri unampenda Mungu, halafu nduguyo unamchukia.</u>**

*1Yohana 4:20 Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona*

**V. <u>Kukiri umeokoka halafu, njia zako zipo mbali na yeye:</u>**

*1Yohana 1:6  Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli; (1Yohana 2:4)*

**VI. <u>Kumpinga Kristo na kazi zake</u>**

*1Yohana 2:22  Ni nani aliye mwongo ila yeye akanaye ya kuwa Yesu ni Kristo? Huyo ndiye mpinga Kristo, yeye amkanaye Baba na Mwana*

Hivyo ombea vipengele hivyo vyote, Ukimsihi sana Bwana aondoe, aina zote za uongo, ndani yako. Omba sana, kwasababu ukitibiwa hapa, utamkaribia sana Mungu kwa viwango vya juu.

## 3) <u>MIKONO IMWAGAYO DAMU ISIYO NA HATIA</u> (Dk 50)

Mikono imwagayo damu, maana yake ni uuaji.  Upo uuaji wa mwilini, lakini pia upo uuaji wa rohoni.

**<u>Uuaji wa mwilini:</u>**

- ✓ Usimuue mwanadamu yoyote.
- ✓ Usitoe mimba, wala usitetee au kushughulika katika tendo hilo ovu.
- ✓ Usitoe huduma/ vitu ambavyo unajua kabisa, vinamadhara au  vinashiriki, kumuangamiza mwanadamu mwenzako.

**<u>Lakini Uuaji wa kiroho ni upi?</u>**

**i) <u>Kumchukia ndugu yako:</u>**

*1Yohana 3:15  Kila amchukiaye ndugu yake ni mwuaji: nanyi mnajua ya kuwa kila mwuaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake*.

- ➢ Mwombe Bwana, akuondolee hasira dhidi ya wanadamu wote.
- ➢ Akuondolee roho za visasi na vinyongo
- ➢ Akupe kuachilia na kusemehe. Hata saba mara sabini
- ➢ Akupe moyo wa huruma
- ➢ Akupe amani na watu wote (Waebrania 12:14)
- ➢ Akupe upendo wa kuwaganga watu moyo zaidi ya  kuwajeruhi. Uwe tabibu kwa wengine sio muuaji.

ii) **<u>Lakini pia uuaji ni kutowashuhudia wengine habari njema, ulizoagizwa na Mungu</u>**.

Ikiwa unayotabia ya kutosema yale Mungu aliyokujalia kwa wengine ili wapone, ukaendelea kimya  hivyo hivyo mpaka watu wale wakafa katika dhambi zao, angali  ilikuwa ni ndani ya

uwezo wako kuwasaidia ujue kuwa hapo ni sawa na umemwaga damu zao, na hivyo Mungu atazitaka mikononi mwako.

*Ezekieli 3:20 "Tena mtu mwenye haki aiachapo haki yake, na kutenda uovu, nami nikiweka kikwazo mbele yake, atakufa; kwa sababu hukumwonya, atakufa katika uovu wake, wala matendo yake ya haki aliyoyatenda hayatakumbukwa; lakini damu yake nitaitaka mkononi mwako. 21 Bali ukimwonya mwenye haki, kwamba yule mwenye haki asitende dhambi, tena ikiwa yeye hatendi dhambi, hakika ataishi, kwa sababu alikubali kuonywa; nawe umejiokoa roho yako".*

Mwombe Bwana akupe nguvu ya kuwashuhudia wengine habari njema. Wala usione aibu au haya, au kudhalilishwa.

## 4) MOYO UWAZAO MAWAZO MABAYA; (Dk 50)

Mawazo mabaya ni mawazo ambayo wakati wote hufikiria mambo yasiyompendeza Mungu.

Kwamfano

**Mawazo ya kizinzi:** Mfano wa haya ni kama yale yaliyomjia Daudi kwa mke wa Huria

**Mawazo ya wizi na rushwa:** Muda wote ni Kufikiri ni kwa namna gani utaiba mali, ufanikiwe.

**Mawazo ya anasa za kidunia**: Wakati wote kuwaza, mambo ya kidunia, miziki, disco, fashion mpya, huna muda na Mungu wako.

**Mawazo ya kujipatia utajiri kwenye kazi ya Mungu :** MFano wa hawa alikuwa ni Yuda**,** Badala ya kufikiri wokovu wa roho za watu, unafikiri ni namna gani utapata mali au faida katika kumtumikia Mungu

**Mawazo ya kujilimbikizia mali na ubinafsi:** Mfano ni Yule mtu aliyefanikiwa akasema moyoni mwake nitavunja ghala zangu, niweke nyingine, nijishibishe kwa siku nyingi. Lakini usiku ule ule akafa.

- ✓ Mwombe Bwana akugeuze kuwaza kwako, kuwe safi, kwa kiasi na kwa kujishusha mbele za Mungu, lakini pia ya kiibada kwa Mungu wakati wote.

## 5) MIGUU ILIYO MYEPESI KUKIMBILIA MAOVU. (Dk 50)

Bwana anataka miguu yetu iwe myepesi kukimbilia matendo mema na sio maovu. Kwamfano pale tunapokuwa radhi kwenda kwenye sinema au mpira tunapoalikwa mara, zaidi ya kwenda kwenye nyumba ya ibada ni chukio kwa BWANA. Tumekuwa wepesi kwa shetani, lakini kwa Mungu ni wazito.

Ombea hivi vipengele;

- ✓ Omba Bwana aifanye miguu yako kuwa myepesi kwenda kanisani
- ✓ Aifanye kuwa myepesi kwenda kuwasidia wengine, wenye shida na mahitaji
- ✓ Myepesi kwenda kwenye vikundi vya maombi na mikesha na wengine
- ✓ Myepesi kwenye ushuhudiaji wa injili.

## 6) SHAHIDI WA UONGO. (Dk 50)

Shahidi wa uongo ni mtu anayetoa ushuhuda wa uongo. Kwamfano umesimamishwa mahakamani, halafu anatokea mtu anasema nilimwona huyu akiwapiga risasi raia 10, wakati wewe hujawahi hata kuijua bunduki ni nini  huo ni ushuhuda wa uongo.

Lakini kinyume chake ikatokea mtu anakushuhudia ukweli utapendezwa sana na mtu huyo. Ndivyo Mungu anavyotaka sisi tuwe mashahidi wa kweli kila eneo tulilopo.

Omba Bwana akusaidie uwe;

i. **Shahidi wa kweli Kwa wanadamu:** Uisimamie haki, wala usiupindishe ukweli Uwapo;
- ✓ Mahakamani
- ✓ Nyumbani
- ✓ Shuleni
- ✓ Kazini

**ii. Shahidi wa kweli Kwa Mungu;**
- ✓ Kwa kuihubiri injili ya kweli isiyoghoshiwa. Yaani kumuhubiri Kristo, sawasawa na Neno lake.
- ✓ Kwa mienendo yetu. Ili Mungu atakukuzwe kwa kupitia sisi
- ✓ Kwa kuwa tayari kujitoa kwa vyote kwa ajili ya Mungu wetu na kwa injili yake.

## 7) NAYE APANDAYE MBEGU ZA FITINA. (Dk 50)

Mbegu za fitina ni matendo ya uchonganishi.  Bwana hapandi tuwe wachonganishi bali kinyume chake tuwe wapatanishi. Maana yake ni kuwa tuwe wapandaji wa mbegu. Lakini sio zile za fitina bali zile za upatanishi.

Hivyo popote uwapo mwombe Mungu, akupe

- ✓ moyo na bidii ya  kuwapatanisha ndugu wanaogombana
- ✓ Kuwapatanisha Ndugu na Kristo ili waupokee wokovu
- ✓ Kuwapatanisha Marafiki marafiki zako na Kristo
- ✓ Kuupatanisha Ulimwengu wote na Kristo.

Bwana akubariki.

Ukizingatia kuombea vipengele hivyo kwa bidii kwa saa zote sita (6). Upo uponyaji mkubwa sana utaingia nafsini mwako. Na hatua nyingine ya juu sana ya utapandishwa,. Maombi! Maombi! Maombi! Ndio kukua kwetu. Usiwe mvivu katika kuomba, shindana, wa nguvu zako zote, jijenge nafsi yako, au muda wako, utumie kuwepo magotini.

Usikose mwendelezo..

Kwa ushauri/ Msaada/ Maombezi wasiliana nasi kwa mawasilino haya;

Na, Mwl Denis & Devis Julius
Nuru_ya_ Upendo
Website: www.wingulamashahidi.org
Email: info@wingulamashahidi.org
+255693036618/ +255789001312